JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA KUMI NA NANE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU

(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)

29 JANUARI, 2015

MKUTANO WA KUMI NA NANE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU

(SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS - THIRD SITTING)

TAREHE 29 JANUARI, 2015

I. DUA:

Dua ilisomwa saa 3.00 asubuhi na Mhe. Spika Anne S. Makinda (Mb) na Kikao kiliendelea.

Makatibu Mezani: 1. Dkt. Thomas D. Kashilillah
2. Ndg. John N. Joel
3. Ndg. Ramadhan I. Abdalah
4. Ndg. Joshua Chamwela

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

Wabunge wafuatao waliuliza Maswali kwa Waziri Mkuu:-

(i) Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe, Mb.

(ii) Mhe. Seleman Said Jafo, Mb.

(iii) Mhe. Mussa Azan Zungu, Mb.

(iv) Mhe. Khalfan Hilary Aeshi, Mb.

(v) Mhe. Stephen Hilary Ngonyani, Mb.

(vi) Mhe. Mohamed Habib Mnyaa, Mb.

III. MASWALI YA KAWAIDA:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa:

1. OFISI YA WAZIRI MKUU:

   SWALI NA. 30: Mhe. Prof. Peter M. Msolla, Mb

   Nyongeza: (i) Mhe. Prof. Peter Msolla, Mb.

   (ii) Mhe. Feeman Aikaeli Mbowe, Mb.

2. OFISI YA RAIS(UTAWALA BORA)

   SWALI NA. 31: Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb.

   Nyongeza: (i) Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb

3. WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO

SWALI NA. 32: Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb.

(ii) Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb.

4. WIZARA YA FEDHA
SWALI.NA. 33: Mhe. Dkt. Hamis A. Kigwangallah, Mb.

Nyongeza: Mhe. Dkt. Hamis A. Kigwangallah, Mb.

5. WIZARA YA NISHATI NA MADINI
SWALI NA. 34: Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiy, Mb.

6. WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SWALI NA. 35: Mhe. Leticia M. Nyerere, Mb. (liliulizwa na Mhe. James Mbatia)

Nyongeza: (i) Mhe. James Francis Mbatia, Mb.

7. WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI
SWALI NA. 36: Mhe. Herbert James Mtangi, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Herbert James Mtangi, Mb

(ii) Mhe. Joshua Samwel Nassari, Mb

8. WIZARA YA HABARI VIJANA,UTAMADUNI NA MICHEZO
SWALI NA. 37: Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya, Mb.

(ii) Mhe. Joseph Mbilinyi, Mb.

V. MATANGAZO:

(a) Wageni wote waliokuwepo katika gallery ya Spika na gallery ya Maafisa walitambulishwa.

(b) Kamati zifuatazo zilitakiwa kukutana saa 7.00 mchana katika kumbi mbalimbali

(i) Kamati yaTAMISEMI – Ukumbi Na. 229

(ii) Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji – Msekwa B

(iii) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira - Msekwa

(iv) Kamati ya Miundombinu – Ukumbi Na. 231.

(v) Kamati ya Ukimwi - Msekwa C.

VI. HOJA YA DHARURA:

- Mhe. Spika, alimkaribisha Waziri wa Mambo ya Ndani ilia toe maelezo ya Serikali kuhusu Hoja iliyotolewa na Mhe. James Mbatia, Mb kuhusu tukio la kupigwa Mwenyekiti wa CUF Taifa, Mhe. Prof. Ibrahim Lipumba.

- Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Mathias Chikawe alitoa maelezo hayo, akielezea tukio lililotokea siku ya tarehe 26/01/2015 jijini Dar es Salaam, ambapo Mwenyekiti wa CUF Taifa na wanachama wengine walidaiwa kuandamana na kufanya mkutano bila kibali, wanadaiwa kupigwa na jeshi la Polisi.

- Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipewa nafasi kuelezea kwamba suala hilo limechukua sura mpya sasa kwa kuwa Prof. Ibrahim Lipumba amefikwisha Mahakama ya Kisutu jana, na kwa hatua hiyo Bunge linatakiwa kuzingatia matakwa ya sheria kwa kutokuzungumzia mambo yanayosubiri maamuzi ya Mahakama. Katika ushauri wake, na kwa kuzingatia matakwa ya kikatiba Mwanasheria Mkuu alishauri kuwa Hoja hiyo ya kujadili jambo la dharura isijadiliwe na Bunge ili kutokuingilia mambo yaliyoko Mahakamani.

- Mhe. Spika, alipokea ushauri wa AG, hata hivyo alikubali hoja hiyo ijadiliwe kwa kila Mbunge kutumia muda wa dakika tatu (3). Uamuzi huo ulipingwa na kambi ya Upinzani na waliendelea kutaka hoja hiyo ijadiliwe kwa dakika (15) kikanuni. Spika alikubali mjadala uendelee kwa kila Mbunge kutumia dakika kumi (10).

VII. WACHANGIAJI:

Waheshimiwa wafuatao walipata nafasi ya kuchangia hoja iliyotolewa na Mhe. James Francis Mbatia:-

(i) Mhe. Tundu Antiphas Lissu, Mb - CHADEMA
(ii) Mhe. Habib Juma Mnyaa, Mb - CUF
(iii) Mhe, Felix Francis Mkosamali, Mb - NCCR MAGEUZI
(iv) Mhe. Joshua Samwel Nassari, Mb - CHADEMA
(v) Mhe. Rashid Ali Abdallah , Mb - CUF
(vi) Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - CUF
(vii) Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe, Mb - CHADEMA
(viii) Mhe.Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mb - CCM
(ix) Mhe. Said Juma Nkumba, Mb - CCM
(x) Mhe. Yahya Kassim Issa, Mb - CCM
(xi) Mhe. Sadifa Juma Sadifa, Mb - CCM
(xii) Mhe. Livingstone J. Lusinde, Mb - CCM

Baada ya kuchangia Mhe.Spika alitoa nafasi kwa mtoa hoja Mhe. James Mbatia ili aweze kuhitimisha hoja yake. Mtoa hoja alihitimisha hoja yake kwa kutumia muda wa dakika kumi na tano (15).

Baada ya mtoa hoja kumaliza, Mhe.Spika, alihitimisha kwa kusema suala hilo litaendelea kufanyiwa kazi na Mahakama, na pia kamati husika ya Bunge italifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuangalia kanuni ya 47 kuhusu mambo ya dharura.

TAARIFA

Naibu Waziri wa Habari alitoa taarifa kuwa TBC hawajakata matangazo siku hiyo.

VIII. KUSITISHA BUNGE:

Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni

IX. BUNGE KUREJEA:

Saa11.00 jioni Bunge lilirejea na kuongozwa na Mhe. Spika.

X. HOJA ZA KAMATI:

Mhe.Spika alianza kuwakaribisha Wenyeviti wa Kamati za Bunge zinazoshughulikia Fedha za Umma kuwasilisha taarifa za Kamati zao kama ifuatavyo:-

(i) Mhe. Kabwe Zubeir Zitto (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali alisoma maoni ya Kamati na kutoa hoja kuwa Bunge lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati hiyo pamoja na maoni na mapendekezo yake.

(ii) Mhe. Rajab Mbarouk Mohammed (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, alisoma maoni ya Kamati na kutoa hoja kuwa Bunge lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati hiyo pamoja na mapendekezo na maoni yake.

(iii) Mhe. Kidawa Hamid Saleh (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti alisoma maoni ya Kamati na kutoa hoja kuwa Bunge lipokee na kuikubali taarifa ya Kamati hiyo pamoja na mapendekezo na maoni yake.

Baada ya uwasilishaji huo, Mheshimiwa Spika alitoa maoni kuhusu umuhimu wa Serikali kujibu hoja zinazotolewa na Kamati za Bunge za PAC na LAAC kwa maandishi, huo ndio utaratibu mzuri wa Kibunge. Kwa sababu hiyo alikaribisha Serikali kujibu na kutoa maelezo kuhusu hoja za Kamati kama ifuatavyo:-

- Mhe. Saada Mkuya Salum (Mb), Waziri wa Fedha alipewa nafasi kutoa maelezo na majibu kuhusu hoja za Mkaguzi Mkuu na Kamati ya PAC.

- Mhe. Hawa A. Ghasia (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, alipewa nafasi ya kutoa maelezo ya ufafanuzi na maoni kuhusu hoja zilizotolewa na Mkaguzi Mkuu pamoja na kamati ya LAAC.

XI. UCHANGIAJI WA HOJA:

Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kuchangia hoja za Kamati hizo tatu za Bunge.

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb - CCM

Mhe. Mwanasheria Mkuu, na Spika walitoa mwongozo kuhusu Wabunge hasa aliekua anachangia Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), kutokuzungumzia suala la UDA kwa kuwa lipo Mahakamani.

XII. KUAHIRISHA BUNGE:

Saa 1.35 usiku Mhe.Spika aliahirisha Bunge hadi kesho Ijumaa tarehe 30/01/2015 saa 3.00 asubuhi.

DODOMA **DKT. T. D. KASHILILAH**